*JINA………………………………………………………. DARASA ……………………….NAMBARI……………….*

# MJARIBU WA KATI YA MUHULA WA PILI, 2025
# KISWAHILI
# KIDATO CHA NNE

Maagizo

1. Jibu maswali yote kwenye karatasi hii
2. Maswali yajibiwe kwenye nafasi zilizoachwa.

**1. UFAHAMU (AL. 10)**

Soma Makala yafuatayo kasha ujibu maswali.

Ama kweli maiasha ya vijana wa kisasa yanatofautuiana na kuhitilafiana pakubwa na yale ya wazee wao. Sio katika mavazi, lugha, mienendo, mitazamo na mielekeo tu bali pia katika kipengele kingine chochote utakachofikiria. Yote haya ni vielelezo vya jinsi kizazi cha leo kinavyoishi katika ulimwengu ambao ni kivuli tu cha ule wa vizazi vilivyotangulia. Baadhai ya watu wameieleza hali hii kuwa maisha sio jiwe. Kwao basi, si ajabu katu kuwa ona vijana wakizungumza lugha yao ya kipekee au wakivaa nguo zinazobana ajabu na kudhihirisha bayana maungo yao badala ya kuyasitiri.

Hata hivyo, watu wengi wameonelea kwamba hali ya maisha ya vijana waleom ni maasia yanayotokana na utundu na hata ukatili wao. Upande huu umetoa rai kwamba kizazi hiki kisingepotoka kama tu kingezingatia na kustahi utamaduni wa wahenga wao ambamo wazazi wao ndimo walimukulia. Wanazidi kufafanua kuwa nyendo hizi za miaka ya nyuma zilithamini san amali kama uaminfu, heshima kwa wazee ama wakuu, bidii, ushirikianao, ukarimu, unyenyekevu, hadhari katika kila jambo, utiifu na pia kujitegemea. Yote haya yamesahaulika ama tuseme yamepuuzwa katika "Utamaduni wa kisasa."

Swali linalizuka sasa ni je, tunapaswa kuwahukumu vijana wa leo kwa kutumia vigezo au masharti gani? Tuwapige darubini kwa kutegemea hali ilvyo hivi leo duniani ama tuwapime kwa mujibu wa jinsi maisha ya baba na babu zao yalivyokuwa. Jibu la sawli hili ni gumu na sharti lifafanuliwe kwa makini lisije likaegemea pande wowote.

Mathalana, ni jambo lisilopingika kuwa maisha ni utaratibu unaothiirika na hivyo kubadilika daima. Angalia kwa mfano jinsi maendeleo ya elimu, sayansi, mawasiliano na hata ufundiyalivyoyageuza maisha siku hizi. Yamkini vijana wa barani Afrika wakaona hata kuzungumza na wenzao kutoka Uropa, Asia na Marikani bila hata kunyanyuka hapa kwao nyumbani. Athari ya filamu, video, vatabu, magazeti, majarida n.k haikadirirki. Haya, kwa kiasi yamewafanya vijana hata kupevuka kabla ya wakati wao. Isitoshe, mambo haya yameweza kuwazuzua na kuwaaminisha kuwa yale wanayojifunza ni kweli. Matokeo yamekuwa ni wao kuudunisha utamaduni wao wa asili na kuupapia ule wa wageni waliowaathiri. Tusisahau kuwa ujana ni tembo la mnazi na rahisi kwao kubadili mawazo.

Lakini hatuwezi kuwasamehe vijana wanaokosa akili razini kwa kupotoshwa na kucharika na yote wanayoyapokea kutoka ugenini na hivyo kuanza kudhalilisha utamaduni wa Waafrika. Hata hivyo, badala ya kuwakashifu wanapopotea njia ama kuwapongeza wanapotenda yale tunayoyategemea tu, ni wajibu mkubwa wa wazazi kuwaongoza na kuwasaidia vijana kuwa na uwezo mkubwa na kufanya uteuzi mwafaka katika maisha yao.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**MASWALI**

A.Kulingana na mwandishi, kundi linalodai kuwa 'Maisha sio jiwe' lina maoni gani? (Alama 2)

- **Lazima maisha yabadilike kwa kutegemea wakati na mwingiliano wa tamaduni.**

B. Kulingana na taarifa ulioisoma ni jinsigani vijana wa kisasa wangeziepuka athari mbaya. (Alama 2)

- **Kwa kuzingatia utamaduni wa wahenga wao ambamo wazazi wao ndimo walimokulia**

C. Kwa mujibu wa taarifa hii, utamaduni wa Kiafrika una manufaa. Yataje, (Alama 2)

**- Uaminifu, heshima kwa wakuu, bidii, ushirikiano , ukarimu, unyenyekevu, hadhari katika kila jambo utiifu na kujitegemea.**

D. Kwa maoni yako vijana wanapaswa kufanya uteuzi wa namna gani katika mvutano huu wa utamaduni? (Alama 1)

**-Wanapaswa kuchagua yale mazuri kutoka kwa utamaduni wa kiafrika na pia kutoka kwa usasa wayafuate, yale yasiofaa wayafutilie mbali.**

E. Eleza msamiati ufautao kama ulivyotumiwa katika Makala (Alama 2)

**i.** Maasia - **Maovu**

ii. Razini – **Tulivu, makini**

F. Andika methali moja ambayo inaafikia taarifa hii. (Alama 1)

**- Usiache mbachao kwa mswala upitao.**
**- Mwacha mila ni mtumwa.**

## 2. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 30)

a. Andika sauti zenye sifa zifuatazo:

a. Irabu ya juu mbele - **/i/**

b. Kipasuo cha kaakaa laini - **/k/ /g/**

b. Huku ukitumia mifano mwafaka, taja aina mbili za silabi. (Alama 2)

- Silabi wazi – **Ka** – **la** – **mu**
- Silabi funge – **Dak** – **tari,** **mak** **- taba**

c. Andika setensi ifuatayo katika hali ya umoja (Alama 2)

Vitabu hivyo vinayaangazia maudhui yaliyoangaziwa katika vile vya kwanza.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Katika hicho kinayaangazia maudhui yanayoangaziwa katika kile cha kwanza.**

d. Andika upya sentensi ifuatayo ikijumuisha vivumishi viashiria vya karibu vya nomino vilivyo pigiwa mstari. (Alama 2)

Mkulima amenunua shamba

- **Mkulima huyu amenunua shamba hili.**

e. Tunga sentensi yenye muundo wa kitenzi halish na kirai kielezi. (Alama 2)

**Baba atasafiri kesho jioni**
**Kitenzi halisi — kirai kielezi**

f. Tumia mtindo wa jedwali kuchaganua sentensi ifuatayo. (Alama 2)

Nitazame nikutazame

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| S1 | | U | S2 | |
| KN | KT | | KN | KT |
| Q | T | | Q | T |
| | Nitazame | Q | | Nikutazame |

g. Akifisha (Alama 4)

musa hakwenda naivasha alisahau kusubiri mpaka alhamisi bakari alisema

**"Musa hakwenda Naivasha, alisahau kusubiri mpaka Alhamisi", Bakari alisema.**

h. Andika katika usemi wa taarifa (Alama 3)

"Anayefuata maaagizo tafaulu mwakani", Musa Alisema.

**Musa alisema kuwa aliyekuwa anafuata maagizo angefaulu mwakani.**

i.Ainisha viulizi hivi (Alama 3)

a. –ngapi - i**dad**i
b. Nini – **kitu/kifaa**
c. Lini **- wakati**

j. Andika kinyume cha: (Alama 2)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Nuna - **Tabasamu**
Hama - **Hamia**

k. Tambua kwa kupiga mstari shamirisho kipozi na shamirisho kitondo katika sentensi zifuatazo. (Alama 4)

i. Faruk alimlimia shamba Halima.
I I
**Kipozi** **kitondo**

ii. Nitampikia mwanangu chakula.
I I
**Kitondo** **Kipozi**

l. Tunga sentensi yeny: (Alama 2)

Kijalizo – **Baba ni mkulima**
**Ali alikuwa nyumbani**

Chagizo – **Wageni watawasili leo jioni**
**Tutaanza mtihani juma lijalo**.

m. Andika katika hali yakinishi: (Alama 1)

Usingeacha masomo usingetaabika vile.

**Ungeacha masomo ungetaabika vile.**

## 3. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

"Naona unaendelea kupata nafuu, utaendelea kutumai dawa hizo hadi uzimalize."

i. Eleza sajili inyatokana na maneno hayo. (Alama 2)

**Sajili ya hospitali/zahanati/kituo cha afya.**

ii.Taja na kueleza sifa zozote nne za sajili uliyotaja. (Alama 8)

a. **Lugha huwa ya kuelekeza**
b. **Lugha ni ya kushauri, mfano, daktari hushauri mgonjwa aina ya vyakula vya kumsaidia.**
c. **Lugha huwa na msamiati maalum, mf. Dawa, daktari, mgonjwa .**
d. **Lugha daktari huwa ya kuhoji ili kujua historia ya ugonjwa.**
e. **Lugha huwa ya matumaini – mgonjwa hupewa matumaini na daktari.**
f. **Lugha huwa ya kuchanganya ndimi, mf. Bp (Blood pressure) iko juu, waerd, Nurse n.k**
g. **Lugha ya pole**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes